HOTUBA YA MKURUGENZI MKUU WA EWURA WAKATI WA TAFTISHI YA HADHARA KUHUSU MAOMBI YA KUONGEZA BEI YA MAJI YALIYOWASILISHWA NA MAMLAKA YA MAJI SAFI NA MAJI TAKA - SHINYANGA (SHUWASA).

17 Mei 2007

Ndugu Waalikwa,
Mabibi na Mabwana

Ninayo furaha kuwakaribisha katika Taftishi ya kwanza hapa Shinyanga kuhusu mapendekezo ya kuongeza bei ya maji yaliyowasilishwa na "**SHUWASA**." Nawashukuru nyote kwa kukubali mwaliko huu uliotolewa kupitia matangazo mbali mbali kwenye magazeti, kwa kutumia vipaza sauti kupitia maeneo mbali mbali na kwa kuwaandikia barua za mwaliko kwa baadhi ya wadau. Mkutano huu ni sehemu ya uchunguzi unaofanywa na EWURA kupata maoni ya wadau wa maji safi na huduma za maji taka kabla ya kutoa maamuzi kuhusu maombi ya **SHUWASA** kuhusu kurekebisha bei. Ni matumaini yangu kuwa maoni yenu katika TAFTISHI hii yatatusaidia kufikia uamuzi mzuri kuhusiana na maombi yao.
Neno Taftishi ni tafsiri ya neno la kiingereza "**inquiry"** lenye maana ya kufanya uchunguzi wa kina juu ya jambo Fulani kabla ya kufanya maamuzi. EWURA kupitia taftishi hii inatafuta maoni ya wananchi na wadau mbalimbali wa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka ya hapa SHINYANGA.

Mabibi na Mabwana;
Tarehe 26 February 2007, EWURA ilipokea maombi ya **SHUWASA** ya kuongeza bei ya maji safi kwa wastani kati ya 38% na 100%. **SHUWASA** inaomba nyongeza hiyo ili iweze kulipia kupanda kwa bei kwa madawa ya kusafishia maji, vipuri, umeme na mafuta. Halikadhalika ongezeko hilo la bei litaisaidia **SHUWASA** kuweza kupanua mtandao wake wa maji na hatimae kuongeza idadi ya

wateja na kuendelea kutoa huduma endelevu kwa wateja. **SHUWASA** iliongeza bei kwa mara ya mwisho mwaka 2004.

Taftishi hii inafanyika ili kupata maoni mbali mbali juu ya uhalali wa **SHUWASA** kuongeza bei ya maji. Wadau wote mnaombwa kuisaidia EWURA kwa kazi hii muhimu kwa kuwa mashahidi wa uchunguzi mzima na kushiriki kwenye taftishi hii kama ratiba inavyoonyesha.

Baada ya kukusanya maoni menejimenti ya EWURA itatoa mapendekezo yake kwa Bodi ya EWURA. Bodi hiyo ndio itakayotoa maamuzi juu ya ombi la **SHUWASA**.

Mabibi na Mabwana;

EWURA ilianzishwa chini ya sheria CAP 414 ya Sheria za Tanzania na imeanza kazi tarehe 20 Februari 2006 kupitia Tangazo la Serikali Na. 19.

Lengo kuu la EWURA ni kuhakikisha huduma ya maji safi na maji taka, umeme, gasi na mafuta zinaimarika kwa kusimamia ubora na bei ya huduma kwa manufaa ya wadau wote na taifa kwa ujumla.

Sheria ya EWURA na sheria za sekta husika zinatoa majukumu yanayotakiwa kutekelezwa na mamlaka. Majukumu hayo ni:

- Kutoa leseni na kusimamia utekelezaji wa masharti yake. Leseni ni mkataba kati ya EWURA na Mamlaka kama **SHUWASA**.
- Kufuta leseni pale inapobidi au kwa mamlaka kama za maji EWURA imepewa uwezo wa kisheria wa kubadili uongozi wa mamlaka ikiwa utakiuka masharti ya leseni.
- Kudhibiti ubora na ufanisi wa utoaji huduma
- Kutathmini na kupitisha bei za huduma
- Kusikiliza malalamiko na kutatua migogoro katika sekta za nishati na maji

- Kuelimisha umma kuhusu shughuli za EWURA

Tangu kuanzishwa kwa EWURA, imefanya mapitio na tathmini za maombi ya mamlaka za maji safi na maji taka za Dar es Salaam, Arusha, Tanga na Singida. Halikadhalika EWURA imefanya mapitio na tathmini ya maombi ya TANESCO na SONGAS ya kufanya mabadiliko katika bei za huduma zake. EWURA ilipitisha maombi hayo baada ya kushirikisha wadau wote wakiwemo watumiaji kama itakavyofanyika leo.

Utaratibu huu wa kukusanya maoni ni katika kutekeleza azma ya Serekali ya utawala bora kwa maana kuwa maamuzi mazito kama haya ni lazima kuwashirikisha wananchi kwa kuwapa fursa ya kutoa maoni yao kwa njia ya uwazi bila kificho.

Awali, udhibiti wa huduma za Nishati na Maji ulikuwa ukisimamiwa na serikali kwa kutumia sheria na mikataba mbalimbali. Mageuzi ya kiuchumi yanayoendelea duniani yanahimiza kuwepo kwa utawala bora, na hivyo kuwepo kwa mgawanyo wa majukumu miongoni mwa Serikali, mdhibiti, na watoa huduma. Uundwaji wa mamlaka za udhibiti kama EWURA ni etekelezaji wa kanuni za utawala bora wenye lengo la kutenganisha majukumu ya kuandaa sera na kusimamia utekelezaji wake kwa upande mmoja, na yale ya udhibiti kwa upande mwingine. Serikali hivi sasa imebaki na wajibu wa kuandaa sera na kusimamia utekelezaji wake, kuwezesha wananchi, na kuhamasisha wawekezaji kushiriki katika biashara na kujenga miundombinu.

Kwa upande wa udhibiti, Mamlaka na Baraza zilizoanzishwa zina wajibu kusimamia sekta husika kwa njia ya uwazi na haki kwa kuzingatia sheria na taratibu zenye kuongeza tija na nafuu kwa pande zote zinazohusika. Mashauriano baina ya vyombo hivi na Serikali yameainishwa katika Sheria. Wizara za sekta husika zina wajibu kutoa maelekezo sahihi ya kisera, pamoja na kutunga sheria mpya au kurekebisha sheria zilizopo.

Mabibi na Mabwana;

Katika kutathmini maombi ya marekebisho ya bei ya huduma, EWURA huzingatia masuala yafuatayo;

- Gharama ya uzalishaji na usambazaji wa huduma husika. Gharama hizo ziwe halali, za haki, kweli na zinazokubalika;
- Urejeshaji wa gharama za uwekezaji;
- Mlinganisho wa gharama za uendeshaji, uwekezaji na viwango vya urejeshaji wa mitaji kati ya **SHUWASA** na Mamlaka zingine za maji hapa nchini zinazotoa huduma zinazofanana.
- Kulinda maslahi ya wateja na wawekezaji.

Mabibi na Mabwana;

Utaratibu wa kupitisha maombi ya kurekebisha bei ya huduma ina hatua kuu saba ambazo zinachukua takribani siku 84 kama ifuatavyo;

- Kupokea maombi;
- Kupitia maombi na kuomba fafanuzi mbali mbali;
- Taftishi ya hadhara;
- Kupokea maoni ya maandishi;
- Kuandaa mapendekezo kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Bodi;
- Maamuzi ya Bodi;
- Kutangaza maamuzi (Agizo) kwenye Gazeti la Serikali na katika magazeti ya kawaida. Katika Agizo hilo, EWURA itaainisha bayana misingi na hoja zilizipelekea maamuzu yake

na masharti ambayo **SHUWASA** itatakiwa kuyazingatia. Baadae agizo hilo litawekwa kwenye mtandao wa EWURA.

Taarifa hizo ni muhimu kwani mtu yeyote asiyeridhika na uamuzi wa EWURA anayo fursa ya kukata rufaa Fair Competition Tribunal.

Mabibi na Mabwana;

Kama nilivyosema mamlaka za udhibiti kama EWURA ni moja ya utekelezaji wa utawala bora. Utawala bora unazingatia misingi mikuu mine na EWURA inaahidi kuizingatia kwa makini. Misingi hiyo ni;

1. **Uwaz**i; Ni kama ambavyo tunazungumza leo na jinsi tulivyowatangazia katika vyombo mbali mbali vya habari na kuweka kila kitu bayana.

2. **Uwajibikaji**; ni kama ambavyo **SHUWASA** leo wamewajibika kwa wadau kwa kuwaonyesha kile wanachofanya.

3. **Kuwa na maamuzi yanayotabirika**; kwa maana ya kuwa mfumo na utaratibu wa EWURA uko wazi na haubadiliki badiliki. Hii hurahisisha mtu kujua matokeo yatakavyokuwa.

4. **Ushirikishaji wadau**; huu ni msingi wa nne. Kama mlivyoona tumewashirikisha wadau, mosi ili mjue kitu gani kinaendelea, pili mje mshiriki na hatimae mtoe maoni yenu.

Mabibi na Mabwana;

Pamoja na maoni yatakayotolewa leo, wadau mnakaribishwa kuwasilisha maoni kwa maandishi kwa;

Mkurugenzi Mkuu,

EWURA, 6th Floor, Harbours View Towers, Samora Avenue,

P.O Box 72175

Dar es Salaam

kabla ya tarehe 31 May 2007 saa 11 Jioni. Maoni yatakayotolewa ndani ya wakati huo yatatumika pia katika kufikia maamuzi ya mwisho.

Mwisho naomba wadau mliopo hapa mshiriki kikamilifu kwa kutoa maoni yenu. Wadau hao ni pamoja na Baraza la Watumiaji wa Huduma zinazodhibitiwa na EWURA na Baraza la Ushauri la Serekali.

Nawakaribisheni nyote na ahsanteni kwa kunisikiliza.